## NAMBA 8: MARKO 11:12-33. MAMLAKA YA YESU

Tayari tumeshaiangalia habari ya kuingia kwa Yesu kwa ushindi, katika **Marko sura ya kumi na moja**, lakini sasa ninawataka tuangalie sura iliyobakia. Hebu tusome **Marko sura ya kumi na moja, mstari wa kumi na mbili, hadi thelathini na tatu**. Katika sura hii, tunamwona Yesu akiulaani mti wa mtini. Tunamwona pia Yesu akilisafisha hekalu, na tunamwona Yesu akiwa akihojiwa juu ya mamlaka haya. Kwa nini viongozi wa Kiyahudi walitaka Yesu auawe? Sababu moja ilikuwa ni kwamba walikuwa na wivu kwa sababu ya umaarufu wake. Sababu nyingine ilikuwa kwamba alidai kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu, na sababu nyingine ni kwa kuwa alitenda na kuzungumza kwa mamlaka.

Neno hilo '*mamlaka*' ni neno lenye nguvu. Kuna hisia ya matumizi ya nguvu kulihusu neno hili, pengine hata hisia ya utisho na hofu. Mtu mwenye mamlaka huwa yuko katika nafasi aliyo-halalishwa; nafasi ambayo unaweza kutekeleza nguvu na utawala; mahali ambapo wana nafasi ya udhibiti na ushawishi. Mtu huyo huwa ana neno la mwisho, na wanaweza kufanya maamuzi juu ya kile kinachotokea katika hali fulani. **Rais** pamoja na serikali za mitaa huwa na mamlaka juu ya maisha yetu. **Polisi** yuko katika nafasi ya mamlaka, na anaweza kuhakikisha kuwa sheria zinafuatwa. **Mwalimu wa shule** ana mamlaka darasani. **Askofu** ana mamlaka juu yenu, linapokuja suala la zima la kazi yako, kama mchungaji au mwinjilisti. Katika mchezo wa mpira wa miguu, **mwamuzi** amepewa mamlaka ya kuhakikisha sheria za mchezo zinazingatiwa. Yeye ni mtu mwenye dhamana ya mechi. Katika kila eneo la maisha yetu, tupo chini ya ‘mamlaka', lakini pia wewe mwenyewe unaweza kuwa katika nafasi ya kuwa na mamlaka.

Lakini - pale tunapojaribu kulinganisha mamlaka ya binadamu yeyote na mamlaka ya Yesu, hakuna ulinganisho. Hakuna mtu hapa duniani ambaye amewahi kuwa na mamlaka kama Yesu, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Yesu alipewa mamlaka na Mungu mwenyewe. **Mathayo sura ya ishirini na nane, mstari wa kumi na nane** inasema hivi: Yesu anazungumza na wanafunzi wake, na kuwaambia, "*Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani*". Katika sura ya kwanza ya **Waefeso**, Paulo anaelezea mamlaka ya Yesu: *"Yeye yuko juu sana kuliko tawala na mamlaka yote, nguvu na mamlaka; Yeye yu juu sana kuliko kila cheo ambacho kinaweza kupewa, sio tu katika ulimwengu wa sasa, lakini pia katika ule ujao - Mungu ameweka vitu vyote chini ya miguu yake".* Mamlaka kamili ya Kristo. Hakuwa na haja ya kujifunza. Hakuwa na haja ya kuyafanyia mazoezi – alipewa na Mungu Baba. Ni haya mamlaka matakatifu ndiyo ambayo yaliwa-kasirisha viongozi wa kidini, hapa katika **Marko sura ya kumi na moja.**

Sasa – tunapotafakari kuhusu mamlaka ya Yesu, utaona kwamba neno '*mamlaka*' imetajwa mara **nne** katika **mstari wa ishirini na saba hadi thelathini na tatu**. Ninafikiri ni vizuri kuyatafakari maneno mawili ya Kigiriki. Neno la kwanza la Kigriki ni '***dunamis***'. Biblia ya Kiingereza inatafsiri neno hili kama '***nguvu***'. Kutokana na neno hilo tunapata neno '*mlipuko*’. Kwa maneno mengine, **dunamis** ni nguvu ya milipuko! Neno la pili la Kigriki ni '***exousia***', na neno hili kwa kawaida linamaanisha '*mamlaka*'. Na ingawa maneno haya yanaweza kutumika pamoja, pia kuna tofauti kubwa. Sikiliza kwa makini, kwa sababu ni muhimu kuelewa aina ya mamlaka ambayo Yesu alikuwa nayo. '**Dunamis**' (nguvu) ni uwezo wa kufanya kitu, wakati '**exousia'** (mamlaka) ni haki ya kufanya kitu.

Kwa hiyo, wakati tunaposema kwamba Yesu alikuwa na mamlaka ya kufanya kitu, tunamaanisha kwamba alikuwa na mamlaka, na uwezo, wa kufanya kitu hicho. Alikuwa na

uwezo wa kuponya wagonjwa na kufufua wafu, lakini pia alikuwa na mamlaka ya kufanya hivyo - alikuwa amepewa ruhusa ya kufanya hivyo kutoka kwa Baba yake. Alikuwa na uwezo na mamlaka. Unaona, sio kila mmoja ambaye ana nafasi ya mamlaka ana uwezo. Fikiria kuhusu hili. Fikiria juu ya **askari polisi** ambaye husimama katikati ya barabara - katika njia panda yenye magari mengi. Kama akitaka kusimamisha gari yoyote, anachotakiwa kukifanya ni kusimama katika barabara, na kuinua mkono wake. Amepewa mamlaka hayo. Ameruhusiwa kufanya hivyo, na sare aliyoivaa pia inampa yeye mamlaka. Hivyo, kulingana na sheria, tunapaswa kutii amri zake. Yeye ana mamlaka ya kusimamisha gari hata likiwa kilometa nyingi! Na kama ukienda Dar utawaona mara nyingi wakifanya hivyo!

Lakini – Je, ana uwezo wa kusimamisha magari? Hapana! Kama dereva akiamua kutosimamisha gari lake, anaweza kukaidi mamlaka yake, na akaendelea kuendesha gari lake. Kwa kweli, hakuna chochote ambacho polisi anaweza kukifanya ili kulisimamisha gari hilo. Anaweza kuwa na mamlaka ya kufanya hivyo - lakini hana uwezo wa kufanya hivyo kimwili. Lakini Yesu – alikuwa na mamlaka yote, na nguvu ya kufanya mapenzi ya Baba. Alikuwa na vyote viwili yaani exousia na dunamis (nguvu na mamlaka) - na ndiyo maana viongozi wa dini hawakupenda hayo. Kwa nini walitaka kumwua Yesu? Ni kwa sababu ya nguvu na mamlaka yake. Lilikuwa ni tishio kubwa katika namna yao ya maisha; hasa kwa kuwa yale mamlaka yake yalikuwa yanavutia usikivu wa maelfu ya watu. Hebu rejea kwenye sura ya kwanza ya Marko. **Sura ya kwanza, mstari ishirini na moja, hadi ishirini na nane:** Yesu anafundisha katika sinagogi huko Kapernaumu. **Mstari wa ishirini na mbili** unasema kwamba: "*Watu walishangazwa na mafundisho yake, kwa sababu aliwafundisha kama mmoja ambaye alikuwa na mamlaka, si kama walimu wa sheria".* Na kisha katika **mstari wa ishirini na tatu**, kuna msukosuko katika huduma. Mtu ambaye amepagawa na pepo mchafu, ghafla alipaza sauti kwa Yesu: "*Tuna nini nawe Yesu wa Nazareti*"? Angalia katika **mstari wa ishrini na tano**. Yesu akamwambia yule mtu: "*Nyamaza kimya! Toka kwake*". Na "*roho mchafu akamtia kifafa, na akalia kwa sauti kuu, akamtoka*". Mamlaka na nguvu yalikuwapo kwa pamoja. Yesu anaamuru – na inatokea. Tunaambiwa katika **mstari wa ishirini na saba**: "*Watu wote walikuwa pale walishangaa, hata wakaulizana wakisema, 'ni nini hii? Ni elimu mpya - na kwa mamlaka! Yeye aweza kuwaamuru hata pepo wachafu wanamtii*".

Na tunajua kutoka katika injili kwamba, Yesu pia ana mamlaka na nguvu wa kuponya magonjwa ya watu. Lakini pia kuna kitu kingine zaidi ambacho Yesu alikuwa na mamlaka ya kukifanya. Katika **sura ya pili** Yesu anamponya mtu ambaye alikuwa amepooza. Mtu huyu alishushwa kupitia darini na marafiki zake, naye Yesu akamponya. Sisi tunaijua habari hiyo vizuri. Lakini, kama vile anavyoweza kumponya mtu kimwili, ana nguvu na mamlaka ya kumponya kiroho pia. Angalia katika **sura ya pili, mstari wa tano**. *"Yesu alipoiona imani yao, alimwambia yule mtu: umesamehewa dhambi zako".* Yesu ana uwezo wa kusamehe dhambi. Na bila shaka viongozi wa dini hawana furaha. Sikiliza kile wanachokisema: *"Yeye anadhani ni nani? Kila mtu anajua kuwa ni Mungu pekee ambaye ana mamlaka ya kusamehe dhambi"?* Na katika **mstari wa kumi** Yesu anaeleza wazi kwamba yeye ana mamlaka ya kusamehe dhambi. Mamlaka na nguvu.

Na kwa kweli, katika kifungu chetu, tunaona kwamba Yesu pia ana mamlaka juu ya vitu vya asili, wakati alipoulaani mtini. Mistari wa **kumi na mbili na kumi na tatu**. Tunaambiwa kwamba walipokuwa wakiondoka Bethania, Yesu aliona mtini kwa mbali. Ni jambo laa kuvutia kutambua kuwa jina '**Bethania**' kweli ina maana ya '**nyumba ya tini**' - hivyo si jambo la kushangaa kwamba walipokuwa wakiondoka kijijini hapo, waliuona mtini. Lakini ni nini mshangao ni kwamba Yesu aliulaani mti kwa sababu ya kutozaa matunda yoyote, ingawa

haukuwa msimu wa tini! Inaonekana kuwa kama si haki juu ya mtini! Kwa nini Yesu aliulaani mti huu wakati ambao si majira muafaka ya kuzalisha tini? Je, Yesu anatumia mamlaka na nguvu kwa njia mbaya, kwa sababu ameudhika kwa kuwa alikuwa hawezi kula matunda? Hapana, sifikiri hivyo. Nafikiri kuna kitu kingine kinachotokea hapa. Yesu anautumia mtini huu kama mfano wa kile kinachokwenda kutendeka katika taifa la Israeli, hii ni kwa sababu mtini mara nyingi, ulitumika katika Agano la Kale kama ishara kwa taifa la Israeli. Kwa hali ya kawaida, wakati wa Pasaka katika Israeli, halikuwa ni jambo la kawaida kuona mti wa mtini, ukiwa na majani mengi. Kwa hiyo Yesu aliuendea ili kuona kama kulikuwa na matunda yoyote. Mti ulionekana ukiwa na afya - lakini hakuwa na dalili ya ya kuwa na matunda yoyote. Labda Yesu anautumia mti huu kulinganisha na hali ya taifa la Israeli. Huenda alikuwa akisema: Israeli inaweza kuonekana ikiwa na afya nzuri; ikiwa imebarikiwa kwa njia nyingi, na ni lazima iwe inazaa matunda. Lakini Israeli haionyeshi matunda yoyote. Kwa hakika, taifa la Israeli ni taifa tasa. Ninaweza kutaja mstari katika Agano la Kale unao-zungumzia pointi hii. **Mika sura ya saba, mstari wa kwanza** – na sikiliza hili kwa makini. Huyu ni Mungu anazungumza miaka **mia saba** kabla Yesu. "*Ole wangu! Maana mimi ni kama mtu anayekusanya matunda ya majira ya joto kwenye shamba la mzabibu, lakini hakuna shada ya zabibu la kuliwa. Mimi ninatamani kula tini, lakini hakuna tini iivayo kwanza".* Na mstari huo unalinganisha vizuri sana na mtini unaozungumziwa hapa katika **Marko sura ya kumi na moja**. Hivyo basi, inawezekana kuwa Yesu anasema: Taifa la Israeli ni kama mtini huu. Halizai matunda yoyote, na kwa sababu hiyo, Mungu ataleta laana juu yake. Na bila shaka, tunajua kwamba katika **mwaka sabini** baada ya Kristo, Yerusalemu uliharibiwa kabisa – kama vile mtini alivyoharibiwa.

Katika **mstari wa kumi na tano hadi kumi na nane** tunaona kwamba, Yesu pia ana mamlaka juu ya hekalu. Yesu ameudhika sana kwa kuwa ibada ya Mungu ilikuwa imeachwa. Watu hawakuwa na dhamira na umakini wa kumwabudu Mungu. Badala jingo la hekalu kutumika kwa ajili ya ibada, hekalu lilitumika kwa ajili ya mambo mengine. Je, unaweza kuifikiria hali na eneo la tukio? Katika hatua hii katika habari hii, kuna watu zaidi ya **milioni mbili** katika Yerusalemu, kwa sababu Pasaka ilikuwa imekaribia. Mji ulikuwa na shughuli nyingi, na kulikuwa na watu wengi ambao walitaka kwenda hekaluni. Eneo wa Hekalu ulikuwa mkubwa sana – ukubwa wake ulikuwa ni sawa viwanja vya mpira wa miguu **kumi na mbili** vikiwekwa pamoja - lakini hata huko katika nafasi hiyo kubwa, kulikuwa na umati mkubwa wa watu.

Kila mwanamume ambaye alitaka kwenda katika eneo la hekalu alitakiwa kulipa kodi. **Kutoka sura ya thelathini mstari wa kumi na tatu** unatuambia kuwa kodi ya hekalu ilikuwa nusu shekeli – na huwezi kutumia fedha yoyote ya kigeni. Kama ulikuwa unatembelea kutoka nchi nyingine, unapaswa kutumia shekeli katika hekalu, kwa hivyo ilibidi uibadilishe pesa yako na kuwa shekeli. Lakini wakati ukifanya hivyo, ulitozwa na kiasi cha ziada, na hiki kilikuwa chanzo kizuri cha mapato kwa makuhani. Watu walikuwa wameweka vibanda vya masoko yao katika viwanja vya hekalu; na siyo ndani ya Hekalu lenyewe, bali ni katika eneo linalolizunguka hekalu. Na watu hawa walikuwa wanauza mifugo, hii ni kwa sababu kila familia ilitakiwa kutoa sadaka ya kondoo katika kipindi cha Pasaka. Kwa hiyo kulikuwa na kondoo na mbuzi wengi wakiuzwa. Kulikuwa na kelele sana! Watu wakipiga kelele, na kubishana kuhusu bei, na kondoo nao pia walipiga kelele. **Mstari wa kumi na tano** inatuambia kuwa Yesu alipotembea katika eneo la hekalu, na akajionea kuwa hekalu lilikuwa linatumiwa vibaya. Yesu alijua kuwa biashara inapaswa kufanyika nje ya hekalu, lakini badala yake, watu hawa walikuwa wanauza vitu vyao ndani ya eneo la hekalu. Na tunaona kwamba Yesu alikasirika sana. Akaanza kuwafukuza wanunuzi na wauzaji. Alipindua meza na mabenchi ya kukalia. Sarafu zote

zilisambaa juu ya sakafu. Uzio wa wanyama ulivunjwa, na kondoo walitoka mbio wakikimbia huku na huku. Yesu amekasirishwa sana na jambo hili. Kwa nini?

Kwa nini Yesu alikasirika? Alikasirika kwa sababu nyumba ya Mungu inatumika kwa ajili ya biashara, badala ya matumizi ya ibada. Je, anasema kitu gani katika **mstari wa kumi na saba**? Ananukuru mstari kutoka **Isaya sura ya hamsini na sita**, na **Yeremia sura ya saba**: *"nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa ajili ya Mataifa, lakini ninyi mmeifanya kuwa pango la wezi".* Miaka **mia sita** kabla Yesu kuja, Yeremia alikuwa amesema kitu kile kile! Mungu alimwambia Yeremia asimame katika eneo la hekalu, na kusema kitu kile kile ambacho Yesu sasa anakisema. Watu wa Kiyahudi katika siku za Yeremia walikuwa wamekumbatia uovu, na ibada zao kwa Mungu zilikuwa tupu na zenye uongo - ni kama tu ilivyo hapa katika Marko sura ya **kumi na moja**.

Unaona, Mungu alikuwa na kusudi na Wayahudi. Aliwataka wawe nuru kwa watu wa Mataifa. Aliwataka wawe mfano wa jinsi ya kumwabudu Mungu. Lakini hapa katika uwanja wa hekalu, ambapo Watu wa Mataifa waliruhusiwa kuingia, Wayahudi walikuwa wamepafanya kuwa "*pango la wezi".* Hapa ndipo watu walikuwa wakijikusanyia pesa. Makuhani walikuwa hata wakinufaika kwa kodi ya hekalu. Ilikuwa ni kelele na machafuko tu. Unawezaje kumwabudu Mungu katika mazingira ya aina hii? Unawezaje kumwabudu Mungu wakati kuna kelele? Unawezaje kuomba mahali ambapo hali yake ni kama ya soko?! Ninafikiri kuna changamoto nyingi kwa ajili yetu hapa. Tunapokutana pamoja siku ya Jumapili asubuhi, Je, tunakutana kumsifu na kumwabudu Mungu kwa heshima? Je, hilo ndilo lengo letu kuu siku ya Jumapili? Au sisi tunakutana ili kufanya majadiliano juu ya kile kilichotokea katika wiki hiyo? Je, tunakutana kufanya biashara na watu wengine? Kama wewe ni mchungaji hapa leo, Je, kanisa lako linatoa fursa kwa Wakristo kuja pamoja, na kumwabudu Mungu katika kweli kwa kupitia sifa na heshima? Vipi kuhusiana na vitu katika maisha yako? Je, kuna vitu katika uwanja wa maisha yako ambayo yanakuzuia kumwabudu Mungu? Au kuna mambo mengi yanayoendelea katika maisha yako – kiasi kwamba huna hata muda wa kumwabudu Mungu?

Unapoketi kanisani siku ya Jumapili, Je, unajali na una umakini katika kumwabudu Mungu, au unajihusisha na shughuli nyingi juu ya kile unachohitaji kufanya katika wiki hiyo? Je, Yesu ndiye kipaumbele maishani mwako? Je, unamruhusu Yesu kuwa na mamlaka katika maisha yako? Chochote ambacho kinatuzuia kumwabudu Mungu, kinatakiwa kuondolewa na kutupwa nje ya maisha yetu, ili ibada ya Mungu wetu iwe katikati. Na labda, hata na kwetu ambao tunafanya kazi katika Kanisa, kuna somo kwa ajili yetu hapa.

Wakati mwingine, kuna hatari kwa wachungaji na wainjilisti. Tumekuwa tukijihusisha na kuangalia saana juu ya biashara na kazi za Kanisa. Mazungumzo yetu yote tunayozungumza ni kuhusu siasa za Kanisa. Yote tunayozungumza ni kuhusu mikutano na vikao vya Kanisa. Tunatumia muda mwingi kuzungumza jinsi ya kuongeza pesa kwa miradi, lakini tunatumia muda mchache katika kumwabudu Mungu! Katika makanisa mengine, matangazo hutumia muda mrefu zaidi kuliko mahubiri! Wakati mwingine sisi tunazingatia sana juu ya kazi za Kanisa, kwa kiasi kwamba mpaka tunasahau kwamba sisi tunakwenda kanisani kwa ajili ya kumwabudu Mungu. Hicho ndicho kinachotokea hapa katika **Marko sura ya kumi na moja**.

Yesu ana hasira. Je, unajua kwamba wakati mwingine ni sawa tu kuwa na hasira? Tunaposoma Biblia tunamwona Mungu akiwa ameikasirikia Israeli katika nyakati nyingi. Baadhi ya watu wanafikiria kwamba mtu hatakiwi kuwa na hasira - lakini hiyo si sahihi.

Mfalme **Daudi**, katika **Zaburi nne**, anasema hii: "*katika hasira yako usitende dhambi".* **Paulo** pia anatumia maneno hayo katika **Waefeso sura ya nne**. Angalia jambo moja kuhusu mstari huo. Mstari hausemi *'kuwa na hasira ni dhambi'*. Unasema kwamba wakati unapokuwa na hasira, hakikisha hautendi dhambi. Tunahitaji kuwa makini hapa. Kuna kitu kama hasira nzuri na yenye haki. Yesu alikuwa na hasira, kwa sababu kile ambacho Wayahudi walikuwa wanakifanya kilikuwa ni cha kumchukiza Mungu. Na wakati mwingine, tunatakiwa kunakili tabia za Mungu, tunaweza kuwa na hasira katika hali fulani. Tunapoona uovu unatokea katika ulimwengu, hatupaswi kuwa kimya; tunapaswa kuwa na hasira. Kama Mungu anapata hasira kwa sababu ya uovu, tunapaswa pia kuwa na hasira wakati tunapoona maovu katika jamii zetu.

Lakini, pia kuna kitu kingine ambacho ni hasira isiyo ya haki. Hiyo ndiyo hasira tunayotakiwa kuwa makini nayo. Tunahitaji kuhakikisha kwamba wakati tunapokuwa na hasira, iwe ni kwa sababu ya kitu ambacho humkasirisha Mungu pia. Tunatakiwa kuhakikisha kwamba wakati tunapokuwa na hasira, hatutakiwi kuwa na kiburi, au chuki, au kulipiza kisasi katika akili zetu. Kwa sababu kama tukifanya hivyo, hasira yetu inakuwa ya dhambi. Usiiruhusu hasira iendelee katika maisha yako kwa muda mrefu, kwa sababu inaweza kuwa tatizo. Inaweza kutusababisha sisi tutende dhambi. Lakini hapa katika Marko sura ya **kumi na moja**, Yesu alikuwa sahihi kuwa na hasira, kwa sababu Mungu amesahaulika. Wayahudi walilitumia hekalu takatifu kama soko. Na wala hawakumheshimu Mwenyezi Mungu. Yesu ana mamlaka ya kulisafisha hekalu. Yeye ana mamlaka ya kuwa na hasira. Yeye ana nguvu na mamlaka juu ya viongozi wa dini - ambao hawawezi kumzuia kufanya hivyo. Hawana nguvu wa kumzuia, katika hatua hii. Kile wanachoweza kukifanya ni kumwangalia Yesu akilisafisha hekalu - na sasa wanaweza kuwa na hasira naye. Lakini hasira yao sio hasira njema, ni hasira ambayo itawasababisha watende dhambi. Walikuwa na wivu, kwa sababu Yesu aliyatia changamoto mamlaka yao. Walikuwa na wivu kwa sababu watu walimpendelea Yesu. Je, matokeo yake ni nini? Angalia katika **mstari wa kumi na nane:** "*wakuu wa makuhani, na walimu wa sheria, walianza kutafuta njia ya kumwua Yesu*".

Mara baada ya tukio hili, huenda siku iliyofuata, Yesu alirudi hekaluni, na tunaambiwa katika **mstari wa ishirini na saba** kwamba '*wakuu makuhani, walimu wa sheria, na wazee walikuja kwake*' wakiwa na swali. Bado walikuwa na hasira sana kwa sababu ya kile kilichotokea katika hekalu. "*Ni kwa mamlaka gani unafanya mambo haya – ni nani aliyekupa mamlaka ya kulisafisha hekalu"?* Ni kitu gani kinakupa haki ya kutufundisha kuhusu mambo ya kiroho? Ni nani aliyekupa ruhusa kufanya, na kuyasema, mambo haya? Unaona, mafundisho ya Yesu yaliwakwaza. Wakati wanapowafundisha watu, wangeweza kunukuu, na kunakili kutoka kwa wanazuoni na walimu wengine. Lakini Yesu hakufundisha kwa njia kama hiyo. Yesu hakuwanukuu walimu wa sheria, Yeye alimnukuu Baba yake ambaye ni Mungu – lakini kwao, hiyo ilikuwa ni kufuru.

Pia, wakati mwingine alikuwa akipingana na kile ambacho Walimu wa Sheria walikuwa wakikisema! Aliweza kusema vitu kama hivi: *'mmesikia imenenwa - mpende jirani yako na kumchukia adui yako, lakini **mimi** ninawaambia kuwapenda adui zenu, na kuwaombea wale wanaowatesa'*. Kwa hiyo alikuwa anapinga kile ambacho Mafarisayo walikuwa wakikifundisha. Alikuwa akisema: Najua kile ambacho viongozi wa dini wamekuwa wakifundisha kwa miaka mingi. Yasahauni mafundisho yao! Fanya kile ninachowafundisha kukifanya! Na hicho kiliwakasirisha! Watu wanasema nini katika haya yote? '*Hiki ni nini*? *Haya ni mafundisho mapya, na anafundisha kwa mamlaka'*! Mafundisho ya Yesu yalikuwa mapya na halisi, wakati mafundisho ya viongozi wa dini yalikuwa ni ya kale na yenye

kuchosha! Mafundisho ya Yesu yalikuwa yanatia changamoto kwa mamlaka ya viongozi wa kidini. Kwa hiyo, waliuliza swali hili: "*mamlaka yako umeyapata kutoka wapi*"? Kwa kweli, Yesu anajua kuwa huu ni mtego. Walikuwa hawana nia ya kweli kupata jibu. Walimtaka tu aseme: *"mamlaka yangu yanatoka kwa Mungu*". Kwa kweli walimtaka yeye aseme hivyo, ili watu waweze kumsikia. Na kisha waweze kuwaambia watu: *"msikilizeni yeye, anaidai kupata mamlaka yake kutoka kwa Mungu".* Na Kisha wangeliweza kumkamata kwa kukufuru na kumpa adhabu ya kifo. Lakini wakati huo alikuwa bado haujafika. Yesu angeamua ni lini jambo hilo lingelitokea. Kwa hiyo Yesu aliwajibu kwa swali. Na kile anachowaambia katika **mstari wa thelathini** ni hiki: *'Yohana Mbatizaji alipata mamlaka yake kutoka wapi'?* Na hivyo viongozi wa dini walikutana pamoja katika kundi na kuanza kuzungumza miongoni mwao.

Lakini, kama unavyoona katika **mistari ya thelathini na moja na thelathini na mbili**, wakagundua kwamba hawawezi kutoa jibu. '*Naam, hatuwezi kusema kwamba Yohana alipata mamlaka yake kutoka kwa Mungu, kwa sababu yeye atatuuliza kwa nini tulimkataa Yohana. Lakini ikiwa tutasema kwamba Yohana alipata mamlaka yake kutoka kwake mwenyewe, watu hawa watasababisha fujo, nasi tutapoteza mamlaka yetu'.* Na hivyo katika **mstari wa thelathini na tatu**, wakati mkutano ulipokuwa unasubiri jibu lao, wakarejea kwa Yesu na kusema: ' *hatujui ni wapi Yohana alipopata mamlaka yake'!* Viongozi wa dini walidhalilishwa! Wakasema "*Hatujui*".

Hivyo Yesu akawaambia, kama ninyi hamniambii ni wapi Yohana alipata mamlaka yake, na mimi pia siwaambii mamlaka yangu yametoka wapi. Ni jibu werevu! Na mafundisho haya-ishii hapo. Kama ukiangalia katika **sura ya kumi na mbili** utaona kuwa Yesu anaendelea kuwapinga viongozi wa kidini. Anawaambia mfano kuhusu wapangaji na shamba la mzabibu. Na mfano huu unawahusu viongozi wa kidini jinsi walivyomkataa Yesu – na walijua kile ambacho Yesu alikuwa akikisema. Nao wakapanga mipango yao zaidi na zaidi ili wapate kumwua. Viongozi wa dini waliasi dhidi ya mamlaka ya Mungu, kwa sababu yanatishia njia yao ya maisha - na hiyo iko sawa kwa watu wengi leo. Tunaishi katika ulimwengu ambapo watu wengi huchagua kuyakataa mamlaka ya Kristo. Na hata kama sisi ni Wakristo, mara nyingi tunaasi dhidi ya mamlaka yake katika maisha yetu. Hebu ngoja niulize maswali machache kwa kadiri tunavyokaribia kuhitimisha. **Kwanza**, Je, ni kweli Yesu ana mamlaka juu ya maisha yako yote? Au kuna baadhi ya sehemu fulani za maisha yako, ambazo bado haujazi-kabidhi chini ya mamlaka yake? Je, Paulo anatuambia nini katika **Barua ya Kwanza ya Wakorintho sura ya sita?** *"Je, hamjui kwamba mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu, aliye ndani yenu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa bei ya thamani".* Kwa maneno mengine, wewe ni mali ya Mungu, na Yeye ana mamlaka juu ya maisha yako. Kwa hiyo, anatuamuru kwamba tujinyenyekeze kwake katika utii.

Na **pili**, kama wahubiri na walimu, iweni imara katika mamlaka ambayo mmepewa katika Kristo. Wewe umepewa mamlaka na Kristo ya kutangaza injili yake katika ulimwengu. Kumbuka maneno haya katika **Mathayo sura ya ishirini na nane**: *"nimepewa mamlaka yote mbinguni na dunia, kwa hiyo kwa sababu ninayo mamlaka hayo, ninawapeni ninyi; Enenda na mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwafunza kutii kila kitu nilichowaamuru".* Watu wanapotuuliza ni kwa mamlaka gani tunaihubiri injili, Je, jibu letu linapaswa kuwa ni lipi? Nina mamlaka ya kuhubiri kwa sababu Kristo amenipatia. Na tunajua kwamba hakuna silaha iliyopangwa dhidi yetu ambayo itaweza kusimama dhidi ya mamlaka hayo. Mamlaka yetu ni dhaifu, lakini mamlaka yake Mungu yana nguvu sana.

------------------------------------------------